# AFRIKA MAGHARIBI






**BASILIKA LA NOTRE-DAME-DE-LA-PAIX (MAMA YETU WA AMANI)LA YAMOUSSOUKRO**

Hili lilijengwa kuinga Basilika la Saint-Pierre (Mtakatifu Petro) la Vatikani. Rais wa zamani wa Côte d'Ivoire, Félix Houphouët-Boigny alilijenga kwenye mji aliozaliwa: Yamoussoukro. Mfano huu unapita jengo la asili kwa kiasi cha mita 20.




**THOMAS SANKARA**

Sankara, ambaye alipewa jina la Che Guevara wa Afrika, alikuwa maarufu kwa mawazo yake ya kisasa na ya kupinga ukoloni. Aliiongoza Burkina Faso hadi kuuawa kwake mwaka 1987. Pia aliibadilisha jina nchi yake, ambayo awali ilijulikana kama "Upper Volta," kuwa "Burkina Faso," maana yake "nchi ya watu wanyoofu" katika lugha ya Kidioula.



**JUMBA LA SANAA KITAIFA**

Jumba la Sanaa la Kitaifa lilizinduliwa mwaka 1976 na ni ishara kwa Wanaigeria. Ni kitovu kikuu cha nchi katika sanaa za maonyesho. Pia ni maarufu kwa kuwafunza waigizaji ambao wamekuwa maarufu katika tasnia ya Nollywood.



**MAJIKEDUME WA DAHOMEY**

Majikedume wa kijeshi hawa walikuwa wapiganaji hodari, walikuwa wakifunzwakuanzia utotoni ili kulinda ufalme wa Dahomey (leo hii nchi ya Benin). Walitekeleza jukumu kubwa katika upanuzi wa eneo la ufalme hadi mwisho wa karne ya 19.



**LA SIERRA LEONE**

Freetown, mji mkuu wa Sierra Leone, uliasisiwa katika karne ya 18 ili kupokea watumwa waliopata uhuru na wafuasi weusi waliounga mkono Uingereza wakati wa Vita vya Uhuru wa Amerika. Mji huo ukawa ishara kwa watu weusi huru, kwani walikuwa huru kuishi hapo.




**MBUYU**

Mbuyu ni ishara ya kitaifa inayoashiria maisha na kifo. Una nafasi muhimu katika utamaduni wa Senegal na katika kuhifadhi bioanuai. Hata hivyo, ukataji miti kwa wingi unatishia kuendelea kuwepo kwake.




**MSIKITI MKUU WA NIAMEY**

Msikiti huu, uliojengwa mwaka 1970 kwa msaada wa serikali ya Libya, una umuhimu mkubwa wa kitamaduni na kidini. Hata hivyo, ni mmojawapo wa misikiti mikubwa katika kanda ya Afrika Magharibi.



**MAKABURI NA BUSTANI YA KUMBUKUMBU YA KWAME NKRUMAH**

Ce mémorial a été érigé en 1992 en mémoire de Kwame Nkrumah, premier président du Ghana et fervent défenseur de l'unité africaine et du panafricanisme. Nkrumah est connu pour avoir joué un rôle crucial dans l'indépendance du pays.



**CESÁRIA ÉVORA**

Evora alikuwa mwimbaji mwenye umaarufu wa kimataifa. Wimbo wake maarufu zaidi "Sodade" fanikiwa sana! Alipewa jina la "Diva wa miguu peku" kutokana na kutojivuna kwake na mara nyingi kupanda jukwaani bila viatu.



**NANAS BENZ (KINAMAMA WA BENZ)**

Wanawake hawa walikuwa wafanyabiashara wa vitenge vya wax (nta), vitambaa vyenye rangi nyingi vinavyothaminiwa sana barani Afrika. Walikuwa nafasi muhimu katika uchumi wa nchi kwa kudhibiti sehemu kubwa ya soko la nguo/vitambaa katika miaka ya 1970 na 1980 na walijipatia utajiri. Pia walijulikana kwa umiliki wao wa magari ya Mercedes-Benz, ishara ya mafanikio yao.



**MITUMBWI YA LEBOU**

Hii ni mitumbwi iliyojengwa kwa kutumia mbinu za kiasili za watu wa Lebou, mbari moja ya Senegal. Hutumiwa na watu hawa kwa uvuvi katika maji ya pwani ya Bahari ya Atlantiki.




**MSIKITI WA DJINGAREYBER**

Jengo hili kubwa la tope ni eneo muhimu sana la kidini na ishara ya usanifu wa Kiislamu, Afrika Magharibi. Mnara wake wa kati, mrefu na unaochukua nafasi kubwa, ni rejeleo la mji wa kihistoria wa Timbuktu.



**WATWAREG**

Hawa ni watu wanaohama-hama wa Sahara walio hasa nchini Niger, Algeria, Libya, na Mali. Mara nyingi huitwa "Watu wa Samawati" kwa sababu ya rangi ya nili wanayotumia kwenye nguo zao.



**MACHO YA SAHARA AU MUUNDO WA RICHAT**

Katikati ya jangwa, kuna muundo wa kustaajabisha uliojengwa na mkusanyo wa mawe na miamba, ambao ukiangaliwa kutoka angani, unachukua umbo la jicho! Kulingana na wanasayansi, ni tukio la zaidi ya miaka milioni 100 iliyopita la kijiolojia litokanalo na mmomonyoko wa udongo ulioendelea kwa muda wa maelfu ya miaka.



**LE LIBÉRIA**


Iliasisiwa mwaka 1822, Liberia ilikuwa koloni iliyolenga kupokea haswa watumwa kutoka Marekani waliopewa uhuru, ambao walikuwa wanataka kurejea Afrika. Mwaka 1847, nchi ilijitangazia uhuru wake, tukio hili likifanya iwe, pamoja na Ethiopia, mojawapo ya nchi chache huru kwenye bara mpaka karne ya 20.



**CHINGUETTI**


Mji wa Chinguetti ulioasisiwa katika karne ya 13, ulikuwa maarufu kwa maktaba zake binafsi nyingi ambazo zilikuwa na maandiko ya kale na maandiko ya kidini ya Kiislamu. Hata hivyo, sasa uwepo wake unatishiwa na uvamizi wa jangwa na hali hii inzidi kuwa mbaya kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Nous remercions tous nos amis de nous avoir aidés à réaliser ce livret.



**FOUTA DJALON**

Hili ni eneo lenye milima ambapo tunaweza kuona vilima vya juu na mabonde yenye vina virefu. Pia ni mahali ambapo vyanzo vingi vya mito vinapatikana nchini Guinea.





**GAMBIA**

Gambia ndiyo nchi ndogo kuzidi zote barani Afrika, yenye eneo la takriban kilomita za mraba 11,300. Ni eneo linalozungukwa kabisa na Senegal. Mto Gambia unapita kuvuka nchi nzima, na kutoa mandhari ya nchi yenye rotuba na utajiri wa bioanuai.



**CHINUA ACHEBE**

Mwandishi na mshairi mashuhuri wa Nigeria, Achebe anachukuliwa kama mmoja wa waanzilishi wa fasihi ya Kiafrika ya kisasa kutokana na riwaya yake ya kwanza, "Things Fall Apart" (Uporomokaji wa Mambo). Maandiko yake hufundishwa katika shule nyingi barani Afrika.




**LA GUINÉE-BISSAU**

Nchini Guinea-Bisau kuna funguvisiwa ya Bissagos , ambayo ni makazi ya watu asilia, wabisago ambayo ni maarufu kwa upinzani wao dhidi ya ukoloni wa Kireno katika karne ya 16 na ya 17 na kwa utamaduni wao wa utaratibu wa mamamkuu.


# AFRIKA KASKAZINI






**MNARA WA HASSAN**

Mnara wa Hassan ni ishara ya Moroko. Ulijengwa Rabat katika karne ya 12, ulikusudiwa kuwa mnara wa msikiti mkubwa zaidi duniani. Hata hivyo, mwaka 1199, mradi huo uliachwa baada ya kifo cha Sultan Yacoub al-Mansour, ambaye alikuwa mwanzilishi wa ujenzi wake.



**MSIKITI WA HASSAN II**

Msikiti wa Hassan II una upande uliojengwa kwenye rasi ya bahari na uko miongoni mwa misikiti mikubwa zaidi duniani! Ndani una upekee wa kuwa na shoroba tatu kuu, zinazoleta taswira ya makanisa makuu, roshani zinazoamsha kumbukumbu za sinagogi, na vigae vya mitindo ya Kiarabu na Kiandalusia.



**PIRAMIDI**

Piramidi ni ishara za Misri ya kale. Zilizo kubwa kuzidi zote zilikuwa zinatumika kama makaburi ya mafarao. Piramidi ya kwanza ilijengwa miaka 4700 iliyopita, na zile maarufu zaidi, kama vile za Khufu, Khafre, na Menkaure, zinapatikana Giza



**TIMGAD**

Kwa jina la utani "Pompeii ya Afrika Kaskazini," Timgad ni mji wa kale wa Kirumi ambao wakati wake uliokuwa tajiri sana. Unapozuru huko, utastaajabishwa na mabaki na magofu yaliyohifadhika vizuri sana na yanayokadiriwa kuwa zaidi ya miaka 2000.



**WAFUMAJI**

Wafumaji wa mji wa Timimoun wanajulikana kwa ufundi wao wa kijadi katika sekta ya kutengeneza nguo/ufumaji, haswa katika ufumaji wa mazulia ya Kiberberi. Wanawake hawa wa hali duni hufuma kwa mikono mazulia haya ya kipekee.



**MSIKITI MKUBWA WA KAIROUAN**

Ni mojawapo ya misikiti ya kale na muhimu zaidi katika ulimwengu wa Kiislamu. Ujenzi wake ulianza karne ya 7, na kadiri miaka ilivyopita, jengo hili limeongezwa na kurarabatiwa.




**AHAGGAR**

Ahaggar ni safu ya milima iliyoko Sahara, ambayo vilele vyake vinafikia takriban mita 3000 juu ya usawa wa bahari. Mahali hapa hutoa mandhari ya kustaajabisha sana, ikiwa ni pamoja na nyanda za juu tambarare kubwa na volkano. Isitoshe, kilele cha juu zaidi nchini Aljeria, Mlima Tahat, kiko Ahaggar.



**CHAI YA MNANAA**

Chai ya mnanaa ni kinywaji muhimu nchini Moroko. Inafurahiwa wakati wowote na kawaida hunywewa kwenye vikombe vidogo.



**ZILIJI**

Ziliji ni sanaa kubwa ya kitamaduni nchini Moroko. Inahusisha kukusanya vipande vidogo vilivyofinyangwa na kuokwa kwenye tanuri ili kutengeneza picha mpangilio. Mapambo haya mara nyingi hutumiwa kupamba kuta katika kasri, misikiti, na makaburi ya kifalme makubwa ili.



**LEPTIS MAGNA**

Leptis Magna ulikuwa mji wa Kirumi ulioko kwenye pwani ya Bahari ya Mediterania. Kwa sasa ni eneo kubwa la akiolojia linaloonyesha usanifu majengo na utamaduni wa Kirumi uliokuwepo zamani Afrika Kaskazini.



**HIIEROGLIFU**

Haya ni maandiko ya Misri ya kale, ya miaka zaidi ya 5000 iliyopita. Maana yake yalikuwa hayaeleweki hadi mwaka wa 1822 wakati Champollion alipofumbua kwa kutumia Jiwe la Rosetta. Jiwe hili ambalo ni kipande cha ubamba wa kale, lilikuwa na maandishi sawa yaliyoandikwa kwa lugha tatu.

*Nous remercions tous nos amis de nous avoir aidés à réaliser ce livret.*

# AFRIKA YA KATI






### MRUNDIKANO WA MILIMA YA TIBESTI

Hii ni safu ya milima ambayo miongoni mwake mna kilele cha juu zaidi nchini Chad na Sahara, Emi Koussi. Kilele hiki kna kimo cha mita 3,415 juu ya usawa wa bahari.



### MAPOROMOKO YA MAJI YA BOALI

Maporomoko haya makubwa ya maji yako kwenye Mto Mbali, karibu na kijiji cha Boali. Yanawakilisha mojawapo ya vivutio vikuu vya utalii nchini. Mabwawa kadhaa ya kuzalisha umeme yamejengwa karibu na maporomoko hayo ili kutoa umeme safi kwa miji jirani na Bangui, mji mkuu wa nchi hiyo.



### LUGHA YA SANGO

Sango ni lugha ya mawasiliano iliyozaliwa katika Jamhuri ya Afrika ya Kati. Ilichaguliwa kuwa lugha rasmi mwaka 1963. Uchaguzi huu unafanya Jamhuri ya Afrika ya Kati kuwa mojawapo ya nchi chache barani Afrika ambazo zimechagua lugha rasmi tofauti na zile zilizowekwa wakati wa ukoloni.



### ZIWA CHAD

Ni mojawapo la maziwa makubwa zaidi barani Afrika. Ingawaje kwa urefu si refu, inapendekezwa kusafiri kwa mtumbwi kwani ziwa chini ni kinamasi. Upana wake unapungua kutokana na tabia-nchi. Wakati wa ukame mkali, inawezekana hata kuvuka katika maeneo fulani.



### SÃO TOMÉ NA PRÍNCIPE

Funguvisiwa hili lililo katika Ghuba ya Guinea, lenye visiwa viwili: São Tomé na Príncipe. Linajulikana kwa bioanuai yake, mashamba ya kakao, na mazingira ya kitropiki.




### MNARA WA SANAMU WA KUMBUKUMBU YA MUUNGANO:

Mnara huu unaadhimisha kuungana kwa pande za Kifaransa na Kiingereza za Kamerun mwaka 1961. Umejengwa kama nyoka wawili wanaokutana na kuungana kwa upande wa juu, kuonyesha muungano wa mikoa miwili iliyokuwa imetengwa awali ili kuunda nchi moja.



### WABORORO

Ni wachungaji wa kuhama-hama. Kwa kiasi kikubwa wanahamahama katika Afrika Magharibi na ya Kati. Wanajulikana kwa uzuri wao mkubwa, wanawake na hata wanaume.



### BONOBO

Bonobo ni aina ya mamalia ya hali ya juu ambayo ni maarufu katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), anayefikiriwa kuwa ndugu wa karibu zaidi wa binadamu. Anajulikana kwa tabia yake ya amani. Hata hivyo, anakabiliwa na hatari cha kutoweka.



### VINYAGO VYA TEMBO

Vinyago hivi hutumiwa na malodi wa Kibamiléké wakati wa sherehe na mila za kitamaduni. Wabamiléké ni watu kutoka eneo la Magharibi wanaofahamika kwa kuzingatia mila za mababu zao na kwa moyo wao wa ujasiriamali.




### EQUATORIAL GUINEA

Nchi hii ina sehemu ya bara na sehemu ya kisiwa. Mji mkuu wake uko kisiwani Bioko. Nchi hii ni mojawapo ya wazalishaji wakubwa wa mafuta katika Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara na ina lugha rasmi tatu: Kihispania, Kifaransa, na Kireno.



### KISUKUKU CHA TOUMAÏ

Kisukuku cha Toumaï kiligunduliwa mwaka 2001 katika jangwa la Djurab. Ni fuvu la mwanadamu wa kale, likirudi kwa takriban miaka milioni 7. Kisukuku cha Toumaï ni babu wa kale zaidi wa nasaba ya binadamu.



### KASUKU WA GABON

Anayetambulika kwa manyoya yake ya rangi ya kijivu, kasuku huyu kwenye misitu ya kitropiki. Anasehemu muhimu kama mchavushaji. Husambaza mbegu na hivyo kuchangia usawa wa mifumo ya ekolojia ya misitu. Mara nyingine hufugwa, ni mwerevu, mwenye shauku, na hasa mzungumzaji.



### VOLANO YA NYIRAGONGO

Mlima Nyiragongo ni volkano hai ambayo ina ziwa kubwa la lava ulimwenguni kote! Mlima unaonekana mara baada ya kutoka kwenye mji wa Goma. Volkano hii inainuka juu ya ardhi nyeusi na yenye rotuba.



### MAKORONGO YA DIOSSO:

Hili ni eneo asilia lililoundwa na Mto Diosso. Makorongo haya huleta mandhari nzuri sana na kuta za mwamba za kustaajabisha na uoto wenye kustawi sana.




### BRAZZAVILLE NA KINSHASA

Brazzaville na Kinshasa ni miji mikuu ya Jamhuri ya Kongo na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ni miji mikuu iliyokaribiana zaidi duniani, iliyotenganishwa na mto Kongo tu.

*Nous remercions tous nos amis de nous avoir aidés à réaliser ce livret.*

# AFRIKA MASHARIKI






### DJIBUTI

Nchi hii inashiriki jina lake na mji wake mkuu: Djibuti. Inajulikana kuwa na tamaduni mbalimbali, ikiwa na makundi tofauti tofauti kama vile Waafar au Waissa.




### WAMAASAI

Ni wafugaji huhama kufuata malisho, waishio kati ya Kenya na Tanzania. Wanafahamika kwa utamaduni wao, mavazi yenye rangi, vito vya kipekee, na maisha yao ya kichungaji. Masai walikuwa pia ni wapiganaji mashujaa waliokuwa wakijulikana kwa ushujaa wao, nguvu na ufanisi.



### NURUDDIN FARAH

Mwandishi huyu wa Kiafrika ni mmoja wa waandishi washawishi wakubwa wa kizazi chake. Katika riwaya zake, anachunguza mada kama utambulisho, ukimbizi, siasa, na jamii ya Kisomali. Kazi yake imetambuliwa na tuzo kadhaa za kimataifa.




### PIRAMIDI ZA NUBIA

Piramidi za Sudan ni nyingi zaidi na za zamani zaidi kuliko zile za Misri. Ziko katika eneo la makaburi ya wafalme na zinahusu ustaarabu wa Nubia. Wanubi ni kundi la mbari ambalo ni miongoni mwa wakazi wa kwanza wa bonde la Nile.



### KAHAWA

Uganda ni mojawapo ya nchi zinazoongoza katika kuuza kahawa ya Afrika, kwa sababu ya hali ya hewa inayofaa na udongo wenye rotuba. Pamba na viazi vitamu pia hulimwa huko.




### MBEGU YA NAZI YA BAHARI

Mbegu hii ni ishara ya Shelisheli. Ni ya mnazi asilia unaopatikana katika kisiwa cha Praslin. Inajulikana kama mbegu kubwa kuliko zote ulimwenguni, na inalindwa kutokana na unadra wake.



### NYAYO ZA LAETOLI

Nyayo za binadamu wa kale ziligunduliwa Laetoli. Zilihifadhiwa katika majivu ya mlipuko wa volkano uliotokea takribani miaka milioni 4 iliyopita. Ugunduzi huu ni muhimu kwa kuongeza uelewa wetu wa enzi za kabla ya historia.



### WAMURSI

Mbari hii inajulikana kwa mila zake za kipekee. Wanawake huvaa miviringo mikubwa ya udongo uliookwa kwenye tanuri ambavyo huviweka kwenye midomo yao ya chini. Miviringo hii huchukuliwa kama kinga dhidi ya mashetani lakini pia kama ishara ya urembo na hadhi.



### MLIMA KILIMANJA-

Mlima huu una kilele cha juu kabisa barani Afrika, kinachofikia urefu wa mita 5,895 juu ya usawa wa bahari. Unajumuisha volkano tatu zilizozimika, na vilele vyake vina barafu. Kwa bahati mbaya, kuyeyuka kwa haraka kwa barafu zake kunavuruga mfumo wa ikolojia wa eneo hilo.



### ZANZIBAR

Kisiwa hiki kilichoko kwenye eneo la bahari la Tanzania kinajulikana kwa mashamba yake ya viungo na fukwe zake za peponi. Historia yake ni tajiri na inachanganya tamaduni za Kiafrika, Kiarabu, na Kihindi.




### BURUNDI

Burundi inajulikana kwa Ingoma, ngoma ya jadi ya nchi. Huchezwa tu na wanaume, ikiambatana na nyimbo na densi wakati wa sherehe za jadi na matukio muhimu.




### HINA

Somalia inajulikana kwa sanaa ya hina, aina ya uchoraji kwenye mwili wa muda unaofanywa kwenye mikono na mara nyingine miguu. Michoro hii hufanywa kutokana na mchanganyiko wa majani ya mmea wa hina yaliyokaushwa na mara nyingi hufanyika wakati wa matukio muhimu kama vile harusi.





### RWANDA

Rwanda imejaaliwa misitu na milima mingi, hivyo basi kupata jina la utani " pays aux mille collines "(nchi ya vilima elfu). Watu wa Rwanda wanajulikana kwa wema na ukarimu wao.




### KIBOKO

Sudani Kusini ni nchi mpya sana, ambayo ilipata uhuru kutoka Sudan mwaka 2011 kupitia kura ya maoni. Nchi hii inajivunia bioanuai ya kipekee: chui, tembo, simba, kiboko n.k.




### ERITREA

Ni nchi iliyoko kando ya bahari Nyekundu. Mji mkuu wake ni Asmara, mji unaojulikana kwa usanifu wake wa kikoloni wa Kiitaliano uliohifadhiwa vizuri. Eritrea ilipata uhuru kutoka Ethiopia mwaka 1993.



### KASRI LA FASILIDAS

Jumba hili la kipekee lilijengwa katika karne ya 17 kwa amri ya mfalme wa zamani wa Ethiopia, Fasilidas. Liko katika mji wenye ngome wa Fasil Ghebbi nchini Ethiopia, ambao una majumba kadhaa yaliyojengwa kwa kuiga mithindo ya Kiarabu, Kihindi, na Kireno.

*Nous remercions tous nos amis de nous avoir aidés à réaliser ce livret.*

# AFRIKA YA KUSINI





**NELSON MANDELA**

Kiongozi huyu alikuwa maarufu ulimwenguni kote na aliongoza harakati dhidi ya ubaguzi wa rangi. Aliendeleza mapambano kwa ujasiri ili kumaliza ukandamizaji wa kiasili nchini Afrika Kusini na alifungwa gerezani kwa miaka 27. Mnamo mwaka 1994, alitawazwa kuwa rais wa kwanza mweusi wa nchi yake.



**WELWITSCHIA MIRABILIS**

Huu ni mmea wa kipekee ambao uota kwenye jangwa la Angola na Namibia tu. Una shina fupi na majani ambayo hukua polepole kwa karne kadhaa, yakifikia upana wa mita 2!



**LA PALANCA NEGRA GIGANTE**

Palahala huyu ni wa kipekee duniani. Anatambulika kwa manyoya yake ya rangi nyeusi na pembe zilizopinda, na ni alama ya taifa la Angola. Kinachosikitisha ni kuwa spishi hii inakabiliwa na vitisho kutoka kwa wawindaji wanaotamani pembe zake.



**JANGWA LA NAMIB**

Ni jangwa la pwani lenye umri mkubwa zaidi duniani, lenye hali ya ukame wa zaidi ya miaka milioni 50. Hapa unaweza kushiriki shughuli za kushangaza, kama vile safari za ndege za kibofu cha hewa!



**WATU WA HIMBA**

Wahimba wanajulikana kwa muonekano wao wa kipekee, haswa wanawake ambao huwa wana mtindo wa nywele wa mabutu yaliyonyooka. Hupaka mchanganyiko wa mafuta ya siagi unga wa rangi nyekundu kwenye nywele. Wahimba huamini kuwepo kwa moto mtakatifu ambao mshumaa wake unaunganisha walio hai na mababu wao.



**WATU WA "SAN"**
**(watu wa mbari kuu ya wawindaji wahamaji)**

Ni mojawapo ya jamii za kale Kusini mwa Afrika, iliyojiasisi takriban miaka 44,000 iliyopita. Hivi leo, Wasan wanakabiliana na changamoto nyingi, kama vile kulinda ardhi yao, kuhifadhi utamaduni wao wa jadi na kukabiliana na utandawazi.




**KOMORI**


Komori ni funguvisiwa lenye visiwa vinne vikuu, yaani Grande Comore, Mohéli, Anjouan, na Mayotte (ya mwisho ikiwa ya sehemu ya Ufaransa). Kila kisiwa kina utamaduni wake, mila zake, na maeneo yake tofauti ya tembelea. Mji mkuu wa Komori ni Moroni, ulioko kwenye kisiwa cha Grande Comore.

**LA RÉUNION**

La Réunion est une île volcanique française réputée pour ses cirques, ses paysages et le métissage de sa population.

**KISIWA CHA MORISI**

Dodo alikuwa ndege muhimu wa nembo wa Mauritius, lakini sasa ametoweka. Kutoweka kwake kunasisitiza umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ili kuhifadhi spishi.





**LESOTHO**

Nchi hii ndogo iko katikati ya bara la Afrika Kusini na inainuka zaidi ya mita 1,400 juu ya usawa wa bahari. Inaitwa kwa jina la "Ufalme angani" kutokana na mwinuko wake na inatoa mandhari ya milima yenye kuvutia sana. Mfumo wa nchi hiyo ni wa ufalme ambapo mfalme ndiye kiongozi wa dola.



**JAHAZI**

Jahazi ni chombo cha jadi kama ngalawa cha asili ya kanda ya pwani ya Afrika mashariki. Hutumiwa kwa uvuvi, kusafirisha bidhaa, na kwa matembezi ya burudani majini. Jahazi la Msumbiji hujulikana kwa tanga lake la pembetatu na mlingoti ulio na vipande viwili. Hutengenezwa na mafundi asilia wenye ujuzi wa jadi.




**ESWATINI**

Nchi hii iko kati ya Afrika Kusini na Msumbiji. Mwaka 2018, Mfalme Mswati III alibadilisha jina la nchi hiyo, ambayo hapo awali ilijulikana kama "Swaziland," kuwa "Eswatini", yaani "nchi ya Waswazi" katika lugha ya Swati kwa lengo la kuimarisha utambulisho wa kitaifa na ikiwa kama ishara ya kujitenga na utawala wa wakoloni wa zamani.



**MAPOROMOKO YA MAJI YA VIKTORIA**

Maporomoko ya maji ya Viktoria yako kwenye mto Zambezi mpakani mwa Zambia na Zimbabwe, ni miongoni mwa miporomoko ya kustaajabisha sana duniani. Je, wajua? Zambia na Zimbabwe ni nchi pekee ambazo majina yake huanza kwa herufi Z!




**ALMASI**

Almasi za kwanza ziligunduliwa mwaka 1866 karibu na jiji la Kimberley, katika jimbo la Northern Cape. Tukio hili lilikuwa chanzo cha historia iliyofanya Afrika Kusini kuwa mmojawapo ya wazalishaji wakuu wa almasi duniani.




**KOMBA**

Hawa ni komba wa usiku, wanaopatikana Madagaska. Katika jamii yao, ni komba wa kike ndio huchukua nafasi ya juu, jambo ambalo ni la nadra sana katika ulimwengu wa wanyama. Kutokana na hilo, komba wanamvutio kama wanyama wenye tabia ya kuchunguza ili kujifunza zaidi.



**MOKOROTLO**

Mokorotlo ni aina ya kofia ya majani, ambayo mara nyingi huvaliwa na mavazi ya jadi ya Sotho. Ni alama ya kitaifa ya Lesotho. Isitoshe, iko kwenye bendera ya nchi hiyo pamoja na kwenye vibambo vya usajili vya gari.




**MALAWI**

Malawi ni nchi ndogo isiyo na pwani iliyoko kati ya Tanzania, Msumbiji, na Zambia. Ina ziwa lenye jina sawa mojawapo wa maziwa makubwa barani Afrika. Nchi huitwa "kiini cha ukarimu cha Afrika" kutokana na ukarimu mkubwa wa watu wake. Mji wake mkuu ni Lilongwe.

*Nous remercions tous nos amis de nous avoir aidés à réaliser ce livret.*